TANGAZO LA SERIKALI Na. 202 la tarehe 17/3/2023

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA)
(SURA YA 287)

# SHERIA NDOGO

*(Zimetungwa chini ya Kifungu cha 153(1))*

MAREKEBISHO YA SHERIA NDOGO YA (HIFADHI YA MAZINGIRA) YA HALMASHAURI YA WILAYA YA NYANG'HWALE YA MWAKA 2023

Jina

TS.Na 324 la tarehe 13/5/2022

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Marekebisho ya Sheria Ndogo ya (Hifadhi ya Mazingira) ya Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale za Mwaka 2023, na itasomwa kwa pamoja na Sheria Ndogo ya (Hifadhi ya Mazingira) ya Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale ya Mwaka, 2022 ambayo hapa imerejewa kama "Sheria Ndogo Kuu".

Marekebisho ya Kifungu cha 3

2. Marekebisho yamefanyika katika Kifungu cha 3 cha Sheria Ndogo Kuu sehemu ya tafsiri kwa kufuta tafsiri ya neno "taka hatari" na badala yake kuingiza tafsiri mpya ya neno hili ili isomeke kama ifuatavyo:

*"Taka hatari" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira.".*

Sura ya 191

3. Marekebisho yamefanyika katika Kifungu cha 3 cha Sheria Ndogo Kuu kwenye sehemu ya tafsiri kwa kufuta tafsiri ya neno *"ardhi hatari.".*

Dodoma,
Machi, 2023

ANGELLAH JASMINE KAIRUKI (MB.),
*Waziri wa Nchi – OR- TAMISEMI*